## Msafiri Yohana Makanta, (1930–2018)

Msafiri Yohana Makanta alikuwa mchungaji wa Kiadventista, mwalimu, mshauri, na mwandishi kutoka Tanzania.

### Miaka ya Mapema

Msafiri Yohana Makanta alizaliwa na kukulia katika kijiji cha Malindi wilayani Lushoto katika mkoa wa Tanga nchini Tanzania mnamo Februari 1, 1930, ambapo baba yake alikuwa mchungaji. Alikuwa wa tatu kuzaliwa kati ya watoto wanne wa familia yao. Mama yake aliitwa Nakijwa Makinya. Makanta alibatizwa mwaka wa 1950 katika kanisa la Waadventista Wasabato Miamba.

### Elimu na Ndoa (1944-1951)

Makanta alijiunga na Shule ya Msingi ya Suji, na kupata cheti cha darasa la nane. Kuanzia 1952 hadi 1953, alijiunga na chuo cha ualimu cha Ikizu (Mara). Baadaye Makanta alijiunga na Chuo cha Bugema nchini Uganda ambako alisomea Diploma ya uchungaji kuanzia mwaka 1956 hadi 1957. Mwaka 1966, alihitimu Diploma ya elimu ya afya kutoka Chuo Kikuu cha Loma Linda cha Public Health and Tropical Medicine Field Station huko Heri Hospital. Mnamo 1971, alipata cheti katika masomo ya kilimo, pia kutoka Chuo Kikuu cha Loma Linda. Julai 7, 1954 alifunga ndoa na Sifael Paul Mweta katika kanisa la Waadventista Wasabato Mamba Miamba wilayani Same mkoani Kilimanjaro nchini Tanzania. Makanta na mkewe walikuwa na watoto watano, John ( Makanta ), Upendo, Stephen, Julius, na Joyce.

### Uchungaji:

Kuanzia mwaka 1954 hadi 1955, Makanta alifanya kazi ya ualimu katika Shule ya Msingi ya Chome. Alikuwa mwalimu na kiongozi wa mtaa katika Kituo cha Misheni cha Mbeya kuanzia mwaka 1958 hadi 1963. Mwaka 1964. Makanta aliwekewa mikono ya uchungaji wakati alipokuwa mkuu wa mtaa wa Tabora. Kuanzia mwaka 1964 hadi 1965, alifanya kazi ya uchungaji katika mtaa wa Tabora. Alihamishiwa mtaa wa Magomeni, Dar es Salaam kuanzia mwaka 1967 hadi 1969. Kuanzia mwaka 1969 hadi 1970, alikuwa Chaplain wa Shule ya Sekondari ya Heri na Hospitali ya Heri ya Kigoma. Mwaka 1971, Makanta alikuwa mchungaji wa mtaa wa Kigoma. Aliteuliwa kuwa mkuu wa idara ya uwakili na huduma binafsi wa Tanzania General Field huko Morogoro mwaka 1972, jukumu ambalo alilibeba hadi 1976. Mnamo mwaka 1977, alichaguliwa kuwa mkurugenzi wa maendeleo ya kanisa, uwakili na walei wa North-East Tanzania Field. Mwaka 1984, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa idara ya Shule ya Sabato wa Union ya Tanzania hadi 1989. Mwaka uliofuata, alichaguliwa kuhudumu kama mwenyekiti wa kwanza wa West Tanzania Field huko Kigoma, jukumu alilotekeleza hadi 1996 alipostaafu.

Baada ya Makanta kustaafu, alirudi nyumbani kwake Mamba Miamba na kuendelea kuongoza katika huduma mbalimbali za kanisa la mtaa. Alipokuwa hai, aliandika vitabu na machapisho kadhaa kama vile KIOO, LIHUBIRI NENO, n.k. Alifariki Juni 15, 2018, katika Kituo cha Afya cha Bwambo, wilayani Same mkoani Kilimanjaro, Tanzania.

**Urithi Aliotuachia:**

Makanta alichangia katika elimu ya Kanisa la Waadventista Wasabato, huduma, na uongozi kwa miaka arobaini na miwili. Machapisho yake bado yanachangia katika malezi na uendeshaji wa kanisa. Wakati wa miaka yake ya kustaafu, alikuwa mkulima wa mfano na mshauri kwa wakulima wengi katika kijiji chake.